

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

610


UALIMU

Muda: Saa 3

Mwaka : 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenyе jumla ya maswali **kumi na nane (18)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na swali **moja (1)** kutoka kila sehemu B, C, D na E.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B, C, D na E zina alama **kumi na tano (15)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Eleza kwa kifupi maana ya Saikolojia.
(b) Bainisha faida tatu za kusoma Saikolojia.
2. Orodhesha sababu nne zinazoweza kuleta mabadiliko ya mtaala.
3. (a) Fafanua tofauti mbili baina ya tathmini endegezi na tathmini tamati.
(b) Ainisha matumizi mawili ya matokeo ya tathmini tamati katika elimu.
4. (a) Fasili neno kujifunza.
(b) Fafanua kanuni tatu za kujifunza kama zilivyotolewa na mwanasaikolojia Edward Lee Thorndike.
5. Taja sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio badala ya binadamu.
6. Bainisha faida nne zinazotokana na mtu mzima kufundishwa kwa kutumia njia shirikishi.
7. Taja mambo manne yanayoweza kuathiri ujifunzaji iwapo wanafunzi watakuwa wengi darasani.
8. (a) Eleza kwa kifupi maana ya Upimaji kama inavyotumika katika Elimu.
(b) Eleza kwa kifupi madhumuni matatu ya Upimaji katika Elimu.
9. (a) Ni nini maana ya Uongozi?
(b) Eleza kwa kifupi mambo matatu yanayotokana na uongozi uliobweteka katika shule za msingi.
10. Ni muhimu kufanya majaribio ya zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia somo la Sayansi kabla ya kuvitumia darasani. Toa hoja nne kuthibitisha usemi huu.

SEHEMU B (Alama 15)

SAIKOLOJIA YA ELIMU

Jibu swali **moja** (1) kutoka schemu hii.

11. Chambua kwa kina vipengele sita vya nyanja ya utambuzi, kisha tunga swali moja kwa kila kipengele.

12. Kwa kutumia hoja sita, eleza jinsi mazingira yanavyoweza kuathiri ukuaji wa mtoto aliye tumboni kwa mama.

SEHEMU C (Alama 15)

MITAALA NA UFUNDISHAJI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

13. Eleza faida tatu na hasara tatu za njia ya maswali na majibu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji,
14. Fafanua faida sita za kutumia njia ya majadiliano ya vikundi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

SEHEMU D (Alama 15)

UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

15. Kwa kutumia hoja sita, chambua umuhimu wa tathmini katika Elimu.
16. “Elimu bila utafiti ni kazi bure.” Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja sita.

SEHEMU E (Alama 15)

MISINGI YA ELIMU

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

17. Kwa kutumia hoja sita, tathmini elimu ya jadi kwa kufafanua sababu za msingi zilizosaidia kumfanya kila mtu aonekane kama ni mwalimu wa mtoto katika jamii yake tofauti na sasa.
18. Eleza kwa kina mbinu sita ambazo mwalimu anaweza kutumia katika kuwafundisha wanafunzi wenyewe vipaji maalum.